# MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZANZIBAR

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) imeanzishwa chini ya kifungu cha 14 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar namba 3 ya mwaka 2015 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2023 kwa lengo la kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo na viwango vya mazingira kwa ajili ya kupunguza uchafu na uharibifu wa Mazingira.

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) inatangaza nafasi moja ya kazi kwa upande wa Unguja kwa wazanzibari wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi hio. Nafasi inayotangaziwa ni kwa kada ifuatayo:-

**1. Afisa Mazingira Daraja la II (Nafasi 1 Unguja)**

**Sifa za Mwombaji**

Mwombaji awe mzanzibari mwenye umri kuanzia miaka 18 na asiyezidi miaka 45 na mwenye elimu ya Shahada ya Kwanza katika fani ya ***Geographical Information System (GIS) and Remote Sensing***/Geographical Information System and Natural Resource Management/Geographical Information System (GIS) kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**Majukumu:**

1) Kutayarisha na kutekeleza mikakati ya kudhibiti, kupunguza na kuondoa uchafuzi/uharibifu wa mazingira.
2) Kushiriki katika kukusanya taarifa za athari zinazosababishwa na uchafuzi na uharibifu wa mazingira.
3) Kushiriki katika kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na mikakati ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira.
4) Kuandaa taarifa za uhifadhi na usimamizi wa mazingira.
5) Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa kimazingira.
6) Kuelimisha jamii juu ya athari zinazotokana na uchafuzi na uharibifu wa mazingira.
7) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na ripoti ya mwaka.
8) Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

**NGAZI YA MSHAHARA-ZPSF– 02**



CamScanner

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

1) Muombaji aambatanishe vivuli vya vyeti vya kumalizia masomo, cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi (Zan ID).

2) Muombaji mwenye vyeti vya vyuo vya nje ya nchi lazima viwe vimebithibitishwa na Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

3) Atakaewasilisha Statement of Result au Progressive Report maombi yake hayatazingatiwa.

4) Muombaji aambatanishe barua ya maombi ya kazi yenye anuwani ya anaepelekewa (Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar S. L. P. 2808) pamoja na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detail C.V) yenye anuani na namba ya simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu.

5) Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Zan Ajira) kupitia anuani https://portal.zanajira.go.tz

6) Muda wa mwisho wa kutuma maombi haya ni tarehe 31/01/2025.

7) Taarifa zaidi zinapatika katika tovuti ya ZEMA (www.zema.go.tz)



CamScanner